BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 18 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

405. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Wananchi wa eneo la Kitogani, jimbo la Paje, walitoa eneo lao kubwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Uhamiaji Tanzania, na wakati wa ufunguzi wa jengo hilo mbele ya Mgeni Rasmi, Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, ilitolewa ahadi

ya ajira za kawaida kama vile ulinzi na usafi kwa wanachi wa Kitogani, ahadi ambayo haijatekelezwa pamoja na kuwa wananchi wa Kitogani walipeleka maombi yao.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea ahadi hiyo isitekelezwe kwa wananchi wa Kitogani.

(b) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa kwa wananchi wa Kitogani.

<u>Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais</u>:

218. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la watu wenye ulemavu kutumiwa kimiradi kwa shughuli za omba omba, hali inayoichafua Zanzibar na utamaduni wake.

Ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na kuwa na sheria madhubuti itakayodhibiti suala la omba omba nchini.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ</u>:

48. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujenzi wa masoko mbalimbali katika Mji wa Zanzibar, ambayo yamewasaidia wafanyabiashara kufanya biashara zao katika mazingira mazuri na yenye usalama wa hali ya juu. Katika Soko la Chuini, kuna changamoto ya baadhi ya sehemu kujaa maji katika kipindi cha mvua, hali inayopelekea kuleta athari ya kimazingira kwa watumiaji wa soko na kusabaisha kupoteza haiba nzuri ya soko hilo ambalo limejengwa kwa ustadi wa hali ya juu.

(a) Baada ya Serikali kuifahamu changamoto hiyo katika Soko la Chuini, je, imechukua hatua gani ya kuitatua.

(b) Je, ni utafiti gani maalumu wa kimazingira uliofanywa kabla ya ujenzi wa Soko la Chuini, hasa ikizingatiwa kuwa eneo lililojengwa ni miongoni mwa maeneo ya maji.

98. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Chuo cha Mafunzo Zanzibar kimekuwa na kazi kubwa ya kuhifadhi na kushughulikia wanafunzi wanaopelekwa kwa ajili ya kurekebishwa tabia zao. Hata hivyo, Chuo hicho kinafanyakazi katika mazingira magumu ya kushughulikia wanafunzi, ikiwemo kuwepo kwa nyenzo duni za usafiri kwa wanafunzi, hali inayopelekea kutokea kwa changamoto mbalimbali ikiwemo kutoroka. Baadhi ya vyombo wanavyotumia ni vya kawaida ambavyo si rafiki kusafirisha wanafunzi kama vile "Townace" na nyenginezo.

Ni lini Serikali itawapatia Vyuo vya Mafunzo vyombo vya usafiri vinavyolingana na kazi zao, ili kuimarisha huduma za usafirishaji wanafunzi na kuepusha changamoto za kutoroka.

**<u>Wizara ya Fedha na Mipango:</u>**

70. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la kutotiliwa maanani suala la kukata bima kwa vyombo vya usafiri vya Serikali. Na kwa kuwa jambo hili ni kinyume na kanuni ya 124(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014.

Je, ni kwa nini Serikali haichukui hatua kwa taasisi zinazokwenda kinyume na Kanuni hizi.

**<u>Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:</u>**

3. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali ilitoa maamuzi ya kubinafsisha Idara ya Usafirishaji na Leseni ambayo ni muhimu katika usalama wa nchi yetu hasa Kitengo cha Kupasisha gari na vyombo vya moto vya magurudumu mawili.

(a) Je, ni sababu zipi zilizoipelekea Serikali kutoa uamuzi wa kubinafsisha Kitengo hicho.

(b) Ni mwekezaji kutoka nchi gani aliyepatiwa kazi hiyo na mkataba wake una thamani ya kiasi gani.

(c) Je, Serikali imefikia uamuzi wa kubinafsisha kitengo kama hicho kilichopo Pemba.

65. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kumekuwa na tatizo la kuzorota kwa huduma za kutoa makontena katika Bandari ya Malindi na Maruhubi, hali inayowapelekea wafanyabiashara kulalamika. Wafanyabiashara wanalipa shilingi 1,180,000 kwa kontena na kontena hilo linatakiwa kupelekwa Maruhubi kushusha mzigo ambako linachelewa kufikishwa. Hali hii inapelekea kufika mwezi huku mfanyabiashara analazimika kulipishwa *"demurrage"* ya dola 40 kwa siku kwa ucheleweshaji ambao wala hahusiki nao.

(a) Je, Serikali imechukua juhudi gani kubaini na kuchukua hatua za kuondoa uzorotaji wa huduma za kutoa makontena katika bandari hizo.

(b) Je, kuna tathmini yoyote iliyofanyika ya kuangalia ubora wa huduma za mwekezaji (ZMT) tokea wapewe zabuni ya kutoa huduma bandarini.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

441. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tatizo la kuzimika umeme kila mara linaleta kero kwa wananchi hasa pale umeme unapozimika bila ya kuwa na taarifa.

Je, kuna mifumo yoyote inayoonesha kukatika kwa umeme na kuwajuilisha wananchi ni maeneo gani umeme haupo ili kuepusha kero na usumbufu kwa wananchi wetu.

## Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

104. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kamisheni ya Ardhi Zanzibar imedaiwa kuchukuwa eneo la mwananchi liliopo Mwanakwerekwe-Mwembedezo, ambalo mwananchi huyu baada ya mgogoro kumalizika Mahakamani, iliamriwa alipwe fidia ya Tsh.210 milioni. Hata hivyo, Kamisheni ya Ardhi imelichukuwa eneo hilo na kuwapa Shirika la Nyumba Zanzibar,

kinyume na utaratibu bila ya kumlipa mwananchi huyu fidia yoyote.

(a) Kwa nini Kamisheni imemnyang'anya mwananchi huyu eneo lake bila ya kumlipa fidia, wakati alishalijenga na wakati anajenga alikuwa na hati kamili.

(b) Kwa nini eneo hilo wamepewa Shirika la Nyumba wakati wenye kulimiliki walikuwa na hati za umiliki ambazo zilifutwa kupisha kazi ya kupitisha umeme ambayo haikufanyika tena baada ya umeme kupitishwa kwengine na ilitakiwa warejeshewe wenyewe au kulipwa fidia.

**<u>Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:</u>**

415. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikijenga viwanja vya kisasa katika maeneo mbalimbali ambayo yalitumiwa na wananchi kufanyiwa michezo mfano viwanja vya Matumbaku, Maisara, Malindi, Mao na vyengine vingi.

Je, ni lini Serikali itavirudisha tena viwanja hivyo mikononi mwa wananchi ili waendelee kuvitumia kama ilivyokuwa awali.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

254. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Jimbo la Mkoani Pemba linakabiliwa na upungufu wa walimu wa sayansi katika skuli zilizomo katika jimbo hilo.

Ni lini Serikali itahakikisha kuwa walimu wa kutosha wa sayansi wanapatikana katika skuli za jimbo la Mkoani ili kukabiliana na changamoto iliyopo sasa.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

378. MHESHIMIWA DKT. MAHMOUD OMAR HAMAD (Jimbo la Tumbatu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua huduma za uchunguzi wa mapema (*screening*) kwa wananchi.

(b) Je, kuna mkakati gani wa kuongeza elimu kwa jamii kuhusu kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza hususani katika maeneo ya vijijini.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

412. MHESHIMIWA MARYAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Kuna ahadi ambayo ameitoa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi ya watu wenye ulemavu kupatiwa mikopo, ili waweze kuendeleza biashara zao. Kwa upande wa Mkoa wa Kusini Pemba, tayari walemavu hao wameshakamilisha taratibu za kujaza fomu kama walivyotakiwa watekeleze.

Je, ni lini watapatiwa mikopo hiyo ili waweze kuendeleza biashara zao.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

222. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Je, ni lini mradi wa kuimarisha eneo la kihistoria la Rasi Mkumbuu Pemba utakamilika.

329. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa Sekta ya Utalii ni nguzo kuu ya mapato ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Na kwa kuwa malipo mengi ya huduma za malazi hufanyika kupitia majukwaa ya kimataifa ya kidijitali kabla ya watalii kufika nchini.

Je, Serikali ina mfumo gani wa kuyasimamia majukwaa ya kimataifa ya kidijitali yanayopata mapato kupitia soko la Zanzibar.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

144. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha bidhaa za baharini kama vile samaki na mazao mengine yanapata masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi ili kuongeza kipato cha wananchi.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

164. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika miaka mingi iliyopita, Zanzibar ilisifika kwa kuuza karafuu nje ya nchi kwa karibu ya asilimia 91, isipokuwa kwamba, kwa miaka ya hivi karibuni, soko la kuuza karafuu nje ya nchi limeshuka kwa kiasi kikubwa;

Je, Wizara ina mpango gani wa kurudisha soko la kuuza karafuu nje ya nchi kama ilivyokuwa zamani.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**18 Mei, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**